

Jarida La Uwezo Tanzania

# TUZUNGUMZE ELIMU

Julai, 2022

Toleo # 0001

Je, Watoto Wetu Wanajifunza?

SIMULIZI ZA MAFANIKIO

## Tathmini ya Uwezo yafanyika Zanzibar



Mapema mwaka huu, **Uwezo Tanzania** imeiongoza taasisi ya **Milelele Zanzibar Foundation (MZF)** kufanya Tathmini ya Uwezo ya kupima viwango vya ujifunzaji kwa watoto visiwani Zanzibar.

Haya ni miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyofikiwa na Uwezo,

katika jitihada zake za kuhimiza wadau wengine Tanzania na hata nje ya eneo hilo, kuichukua Tathmini hiyo na kwenda kupima Uwezo wa ujifunzaji wa watoto katika maeneo yao.

Ili kufanikisha zoezi hilo, Uwezo iliendesha mafunzo juu ya mchakato wa tathmini ya Uwezo na Uandaaji wa

zana ambapo jumla ya wataalamu 14 wa masuala ya elimu waliweza kuhudhuria wakiwemo wafanyakazi wa MZF, Taasisi ya Elimu Zanzibar na shirika la SAZAN. Wakati wa mafunzo MZF walisaidiwa kuandaa muongozo wa misingi ya tathmini bora kulingana na mazingira yao, majaribio ya masomo yatakayo fanyiwa tathmini (Kiswahili, Kingereza

na Hisabati). Baada ya mafunzo hayo, zoezi la kufanya tathmini lilitokelezwa na kufikia zaidi ya kaya 3000 katika wilaya zote 11 za Zanzibar. Hii ni mara ya kwanza tathmini hiyo kufanywa visiwani humo. Ripoti ya tathmini hiyo inatarajiwa kuzinduliwa mwaka huu.

## Walimu wasimulia mafanikio ya mradi wa Jifunze(TaRL)

Baada ya Shirika la Uwezo Tanzania kufuatilia mrejesho toka kwa walimu juu ya mafanikio ya mradi wa Jifunze uliotekelezwa katika wilaya sita (Chamwino, Kisarawe, Mvomero, Ludewa, Kilolo na Mbarali) kuanzia mwaka 2019-2021, walimu wasimulia mafanikio yake huku wakiahidi kuendelea kuzitumia mbinu hizo muhimu katika kuwasaidia watoto kujifunza.

Mwalimu, Vadiana Sanga toka wilayani Mvomero aliambia Uwezo kuwa Jifunze imewasaidia sana kupunguza

idadi kubwa ya watoto ambao walikuwa hawajui kusoma na kuhesabu.

“Baada ya kuja kwa mradi wa Jifunze toka shirika la Uwezo Tanzania tuliweza kuwasaidia watoto wengi waliokuwa na changamoto hiyo kumudu stadi muhimu za kusoma na kuhesabu, tena kwa muda mfupi”, alisema.

Aidha, mwalimu Sanga alisema kuwa, bado wanaendelea kuzitumia mbinu za Jifunze na kuwasaidia watoto wote kuji-

funza.

Sambamba na hilo, walimu wengine, Fatuma Matumla na Christian Sinkonde toka wilaya ya Kisarawe, walisema Jifunze iliwasaidia wanafunzi kuweza kujua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa haraka.

Uwezo inaendelea ku-shirikiana na wadau wengine wa Elimu kutekeleza mradi wa Jifunze ambao umeonesha mafanikio makubwa katika kuinua elimu kwa watoto nchini.





## Uwezo, Milele Zanzibar watekeleza tathmini ya stadi za maisha na tunu

Tathmini kubwa ya kupima stadi za maisha na tunu kwa vijana wenye umri wa miaka 13-17 imefanyika nchini Tanzania kwa mara ya kwanza.

Stadi hii iliyoanza kutekelezwa kuanzia mwezi Aprili na kukamilika Julai mwaka huu, imefanywa kwa ushirikiano wa shirika la **Uwezo Tanzania** na

**Milele Zanzibar Foundation** na imezifikia wilaya 34 za Tanzania bara na takribani kaya 13,600 zimefikiwa na stadi hii katika wilaya hizo.

Ripoti ya tathmini hii inatarajiwa kukamilika na kuzinduliwa mwishoni mwa mwaka huu.

Aidha, stadi hii ilisimamiwa na mashirika wadau wa Uwezo kutoka katika wilaya zote 34 ambapo kabla ya kuanza kazi walipatiwa mafunzo muhimu ili kulielewa vyeema zoezi hilo.

Stadi zilizopimwa wakati wa tathmini hiyo ni kujitambua, kutatua matatizo na ushirikiano na tunu ya heshima.

Kwa maoni wasiliana na mhariri kwa anuani:-  
Uwezo Tanzania  
S.L.P. 8259 Kinondoni,  
Dar es salaam.

Mitandao ya Kijamii  
Twitter: @UwezoTanzania  
Barua pepe:  
info@uwezotanzania.or.tz

Tovuti :  
www.uwezotanzania.or.tz

JARIDA HILI HUANDALIWA  
NA KUSAMBAZWA NA  
SHIRIKA LA UWEZO  
TANZANIA

## MAFUNZO KWA WAJUMBE WA KAMATI ZA HUDUMA ZA JAMII ZA VIJJI



# Uwezo na Jamii yaleta matokeo makubwa Handeni na Gairo

Kupitia programu ya Uwezo na Jamii iliyotekelezwa na shirika la Uwezo Tanzania katika wilaya za Handeni na Gairo kwa mwaka 2021, shirika la Uwezo Tanzania limejionea matokeo mazuri yaliyosababishwa na utekelezaji wa mradi huo katika wilaya hizo.

Kupitia utekelezaji wa mradi wa Uwezo na Jamii, Uwezo iliweza kutoa hamasa kwa wazazi kushiriki katika elimu ya watoto wao, pamoja na kufanya mafunzo ya kuwajengea Uwezo juu ya ma-

jukumu yao, wajumbe wa Kamati za Huduma za Jamii za Vijiji (zaidi ya wajumbe 450 walijengewa Uwezo), imeripotiwa na wadau wa Uwezo waliopo wilayani kuwa, jitihada mbalimbali zimeweza kufanywa na wanajamii ikiwa ni harakati za kutatua changamoto za ujifunzaji na kuboresha elimu ya watoto.

"Mafunzo ya Uwezo yametufanya tuwe makini zaidi katika kuwafuatilia wananchi na kusimamia sheria za serikali, mfano kusimamia wazazi

kuhakikisha kila mtoto anaenda shule" Alisema Abdalla, Mwenyekiti wa Kijiji wilayani Handeni.

Miongoni mwa mambo yaliyotajwa kufanyika ni;- Kujengwa kwa madarasa zaidi ya 16, vyoo 33, na pia zaidi ya shule 21 zimeanza kutoa chakula cha mchana kwa watoto.